

**Issue no:** 01 | **Vol no:** 06 | **September** 2025: 56-64

# Mchango wa Mikakati ya Upole Katika Mazungumzo ya Ibada ya Mazishi katika Lugha ya Kikabarasi

**Simon Peter Katui**

University of Nairobi, Kenya
Main author's email: simonkatui15@gmail.com

**Article History**
Received: **2025.07.14**
Accepted: **2025.08.13**
Published: **2025.09.15**

**Cite this article in APA**
Katui, S. P. (2025). Mchango wa mikakati ya upole katika mazungumzo ya ibada ya mazishi katika lugha ya Kikabarasi. *Editon consortium journal of Kiswahili*, *6*(1), 56-64. https://doi.org/10.51317/ecjkisw.v6i1.623

**Ikisiri**
Suala la upole limetafitiwa na wasomi wengi kwenye mawasiliano, ikiwemo mazungumzo ya abiria na wahudumu wa magari ya uchukuzi kwa lugha ya Kikamba. Hata hivyo, utafiti huu haukuweka wazi udhihirikaji na matumizi ya mikakati ya upole katika muktadha wa ibada ya mazishi katika lugha ya Kikabarasi na umuhimu wake kwenye mawasiliano. Makala hii inachunguza udhihirikaji, matumizi, sababu, na umuhimu wa mikakati hii ya upole kwenye hafla za mazishi. Utafiti huu uliongozwa na nadharia ya Brown na Levinson (1987). Sampuli ilichaguliwa kimakusudi kutoka hafla kumi na tano za ibada ya mazishi katika kitongoji cha Namanja, eneo bunge la Malava, Kakamega, kwa kuzingatia lugha ya Kikabarasi ikilinganishwa na Kiswahili. Usemi wa wanenaji wa hirimu zote, bila ubaguzi wa jinsia, ulirekodiwa kwa idhini ya utawala wa kijiji na kuwekwa katika kategoria za mikakati ya upole kama ilivyopendekezwa na Brown na Levinson. Matokeo yanaonyesha wazungumzaji hutumia mikakati ya upole, hasa mkakati hasi na mkakati nje ya rekodi, kwa sababu za kunasa hisia za wasikilizaji na kuhifadhi sitara zao, hasa waliofiwa, bila kudhuru sitara zao. Utafiti huu utawezesha wasikilizaji na waombolezaji kupata maarifa na ustadi katika kuwahutubia watu wa tabaka mbalimbali katika jamii changamano, na kuongeza data kwa uga wa isimu. Unapendekeza uchunguzi zaidi wa changamoto za mikakati ya upole katika mawasiliano, hasa katika sherehe ya kumbukumbu ya mashujaa na Jukwaa la Facebook.

**Maneno muhimu**: Kabarasi, mikakati ya upole, sitara, wajane.

Editon OPEN ACCESS

This article is distributed under the license of a Creative Commons Attribution-Non Commercial-ShareAlike 4.0 International License. It is permitted to be used, reproduced and distributed in line with Editon Consortium Publishing guidelines.

## UTANGULIZI

Katika lugha ya kimazungumzo, watu hutumia upole kwa sababu ya kuwa na ujumi mzuri au kujinadhifisha na kuleta mwamana kwa wengine, haswa sana wasikilizaji. Upole ni suala bora linalotumika vyema kama njia ya kuonyesha hulka njema. Hii inamaanisha kwamba upole ni jambo ambalo linasheheni mazungumzo kwani linatokeza mitazamo ya mtu kwa wengine. Mitagusano ya kijamii baina ya watu ni jambo ambalo linatokea mara kwa mara kwa aushi ya mwanadamu. Ukosefu wa masomo kuhusu upole katika muktadha wa mazungumzo ya ibada ya mazishi, hususan katika lugha ya Kikabarasi, unasababisha mwanya wa kiusomi kwani iwapo mtu atahitaji kuheshimiwa na kutambuliwa na wasikilizaji katika muktadha wa mazungumzo ya ibada ya mazishi, basi sharti atagusane kwa matumizi ya upole chanya, na iwapo hahitaji kutambuliwa na kuheshimiwa na jamii hiyo, atawasiliana kwa matumizi ya upole hasi ili achukuliwe namna alivyo.

Mikakati chanya ya upole hutumika kwa sababu za kupata majibu chanya kutoka kwa wasikilizaji na kujipatia muonekano mzuri katika mlahaka wa unenaji. Watu hutumia mikakati chanya kimawasiliano kwa ajili ya kutengeneza na kuhifadhi uhusiano mwema katika jamii ya wasikilizaji. Mikakati ya upole kiujumla ni mikakati ambayo wawasilianaji hutumia kwenye mawasiliano ili kuwezesha mawasiliano, aidha kwa kuwafurahisha, kuwatumbuiza, na kuwachekesha wasikilizaji kwa kukwepa kuhasiri sitara zao. Utafiti huu umezingatia suala la upole katika ibada za mazishi ili kubaini mchango wake katika mawasiliano ya lugha za Kiafrika, hasa lugha ya Kikabarasi, pamoja na kutambua mikakati ya upole inayosheheni mazungumzo ya ibada za mazishi na sababu zake za kimatumizi. Nadharia ya upole ya Brown na Levinson (1987) iliegemezwa katika muktadha wa mazungumzo ya ibada za mazishi ili kufanikisha uchanganuzi wa udhihirikaji wa mikakati ya upole, umuhimu wake, na sababu za matumizi yake katika mawasiliano ya mazishi katika lugha ya Kikabarasi.

## MAPITIO YA MAANDISHI

Hadi sasa, suala la upole limechunguzwa na wanazuoni mbalimbali kwa kutumia nadharia ya upole ya Brown na Levinson (1987) ili kuchanganua jinsi mikakati ya upole inavyotumika katika mawasiliano. Kioko et al. (2021) walichunguza mikakati ya upole katika mawasiliano baina ya wahudumu wa magari ya uchukuzi na abiria katika lugha ya Kikamba, ambapo ilibainishwa kuwa wahudumu wa magari na abiria hutumia mikakati ya upole wa chanya zaidi kuliko mikakati mingine ya mawasiliano. Utafiti huo ulichangia sana kwa kubaini matumizi ya mikakati ya upole katika mawasiliano, ingawa unatofautiana na utafiti huu ambao unazingatia mchango wa mikakati ya upole katika mazungumzo ya ibada ya mazishi katika lugha ya Kikabarasi.

Njambi (2010) alichunguza matumizi ya mikakati ya upole katika lugha ya Kikuyu na kubainisha kuwa Wakikuyu hutumia mikakati yote minne ya upole katika mazungumzo yao kwa lengo la kukidhi mahitaji ya kibiashara. Utafiti huo ulisaidia kwa kutoa maelezo kuhusu jinsi mikakati ya upole inavyotambuliwa katika mazungumzo, japo haukuonyesha umuhimu wa mikakati hiyo katika matumizi yake. Muge (2018) alichunguza jinsi mikakati ya upole inavyojitokeza katika vipindi vya redio na kugundua kuwa mikakati ya upole wa chanya ndiyo inayotawala mazungumzo ya wazungumzaji ikilinganishwa na mikakati mingine ya upole. Utafiti huo utachangia katika uchanganuzi huu kwa kutoa uelewa wa matumizi ya mikakati ya upole na kuwezesha tathmini ya matumizi ya mikakati hiyo katika usemi wa wazungumzaji katika ibada ya mazishi kwa lugha ya Kikabarasi.

Adewale (2018) alishughulikia mikakati ya upole inayotumiwa na matabibu katika harakati za kuwahudumia wagonjwa katika hospitali ya chuo cha *Ibadan*, Nigeria, kwa kuchunguza jinsi matabibu wanavyowasiliana na wagonjwa ili kuepuka kuharibu sitara yao. Ilibainishwa kuwa matabibu hutumia lugha ya taadhima na unyenyekevu pamoja na kufanya urafiki na wagonjwa wao kwa lengo la kupata habari kamili kuhusu maumivu ya wagonjwa. Pedzisai (2001) alidai kuwa wafanyakazi wa usafiri wa umma katika mji wa Harare hutumia maneno ya taadhima bila ulazima kwa wasafiri. Utafiti huo unachangia sana kwa kubaini mikakati ya upole katika mawasiliano, ingawa ulizingatia lugha ya Kishona, tofauti na uchanganuzi huu unaozingatia lugha ya Kikabarasi inayopatikana magharibi mwa Kenya. Utafiti wa awali ulishughulikia miktadha tofauti kama vile magari ya uchukuzi, redio, hospitali, lugha ya

Kishona, na lugha ya Kikuyu bila kuhusiana moja kwa moja na muktadha wa lugha ya Kikabarasi. Hata hivyo, makala haya yanatoa maelezo kuhusu mchango wa mikakati ya upole katika mazungumzo ya ibada ya mazishi katika lugha ya Kikabarasi.

**Msingi wa Nadharia**

Nadharia ya upole iliyoasisiwa na Brown na Levinson (1987) imetumika kama msingi wa utafiti huu. Nadharia hiyo ilitambua na kutumia mawazo ya Goffman (1967) kuhusu sitara za binadamu, ambapo kila mwanadamu anasitara mbili: sitara chanya na sitara hasi. Kulingana na Goffman (1967), sitara ni thamani ambayo kila binadamu anayo na ambayo inapaswa kuhifadhiwa katika kila muktadha wa mazungumzo. Brown na Levinson (1987) walizingatia mawazo ya Goffman na kuibua nadharia ya upole, ambapo ilibainishwa kuwa katika mawasiliano ya kila siku, sitara za wawasilianaji zinapaswa kuhifadhiwa ili kufanikisha mapatano na maelewano katika mawasiliano. Mikakati ya upole iliyotajwa katika nadharia hiyo inajumuisha mikakati ya upole wa chanya, mikakati ya upole hasi, mikakati ndani ya rekodi, na mikakati nje ya rekodi, ambayo inatumika kuwezesha uhifadhi wa sitara za wawasilianaji.Mikakati hiyo ya mawasiliano imezingatiwa katika utafiti huu ili kubainisha uelewa kamili wa matumizi ya upole katika lugha ya Kikabarasi na kutambua mikakati inayotawala mazungumzo ya ibada ya mazishi katika lugha hiyo. Nadharia ya upole iliegemezwa katika muktadha wa mazungumzo ya ibada ya mazishi, na hivyo ilifanyika uchanganuzi kamili wa mchango wa mikakati hiyo katika mazungumzo ya ibada ya mazishi katika lugha ya Kikabarasi.

**MBINU ZA UTAFITI**

**Ukusanyaji wa Data**

Utafiti huu umezingatia mbinu za uchunguzi kwa kuhudhuria ibada za mazishi ili kusikiliza mazungumzo moja kwa moja. Katika mchakato wa ukusanyaji wa data, idhini ya wakuu wa mitaa na waombolezaji ilipatikana kabla ya kuwahoji. Mahojiano yalifanyika kwa watu waliokubali kuhojiwa kwa hiari bila kulazimishwa katika ibada za mazishi, bila kuzingatia jinsia, ili kupata picha kamili ya matumizi ya mikakati ya upole katika muktadha wa mazungumzo ya matanga. Sampuli ya utafiti ilichaguliwa kimakusudi, ambapo data ilikusanywa kutoka kwa hafla kumi na tano za ibada ya mazishi, ikizingatia wanenaji wa rika zote bila ubaguzi wa jinsia katika hafla zilizotumika kama sampuli.

**Ufasiri na Uchambuzi wa Data**

Usemi wa wanenaji ulirekodiwa na kuainishwa katika kategoria za mikakati ya upole kama ilivyopendekezwa na Brown na Levinson (1987) katika nadharia ya upole. Data ya mazungumzo ilinakiliwa na kutafsiriwa kutoka lugha ya Kikabarasi hadi lugha ya Kiswahili. Data ilichambuliwa kwa misingi ya nadharia ya upole, na mikakati ya upole ilitambuliwa jinsi ilivyotumika, pamoja na kutoa maelezo kuhusu mchango wake katika mazungumzo ya ibada ya mazishi katika lugha ya Kikabarasi.

**MATOKEO YA UTAFITI**

Matokeo ya utafiti huu yamewasilishwa kwa kuzingatia mikakati minne ya upole: mikakati ya upole wa chanya, mikakati ya upole hasi, mikakati ndani ya rekodi, na mikakati nje ya rekodi, kulingana na nadharia ya upole ya Brown na Levinson (1987).

**Mikakati chanya ya Upole**

Kulingana na Brown na Levinson (1987), mikakati ya upole wa chanya inalenga kuhifadhi sitara za wasikilizaji na kuendeleza mahusiano mema kati ya wawasilianaji katika mawasiliano. Mikakati hiyo ya mawasiliano ilichambuliwa jinsi ilivyojitokeza katika mazungumzo ya ibada za mazishi kwa lugha ya Kikabarasi, na mchango wake katika mazungumzo ya hafla za mazishi ulitathminiwa.

**Matumizi ya mikakati chanya ya upole kwa nia ya kutambulika na kukubalika**

Kulingana na Brown na Levinson (1987), usemi usio na maelewano au ukubalifu unaweza kuharibu sitara za wazungumzaji na wasikilizaji. Mzungumzaji anaweza kuharibu sitara yake kwa kufedheheka au kuaibika katika muktadha wa mazungumzo, huku msikilizaji akijiona amedunishwa kwa kuambiwa mambo yasiyomfurahisha. Kwa hivyo, mazungumzo yanapaswa kujumuisha mikakati ya upole wa chanya ili kufanikisha maelewano yanayowaweka sawa wazungumzaji na wasikilizaji, na hivyo kuhifadhi sitara zao.

**Mifano kutoka kwa mazungumzo ya ibaada za mazishi**

**Mfano wa kwanza:**

**Kikabarasi**

*Omwana wefu vanga Baba nende Vanga Mama vanje, avami veshivala shiefu shino. Mlembe vosi? mulembe khandi? neshivela*

*eshikali sana mungo mno sichila khutifiye eying'ombe ya mavele yikona akari mutsindi.*

**Ufafanuzi**

Mzungumzaji anajinadhibisha na familia iliyopoteza mmoja wao kwa kutanguliza hotuba yake na kutambulisha itifaki kama mmoja wa familia kwa maneno, "Mtoto wetu, baba zangu na mama zangu, hamjambo? Hamjambo tena? Ni huzuni mkubwa sana kwa sababu tumempoteza ng'ombe wa maziwa ambaye ni kiungo cha kati." Mnenaji analazimika kutumia usemi kama huu kwa nia ya kupata ukubalifu ili aweze kusikilizwa na hivyo kupata fursa ya kufikisha ujumbe wake kimawasiliano.

Matumizi ya mkakati huu wa upole yanawezesha ukubalifu kwa mzungumzaji kwani, waliofiwa wanamuona kama mmoja wao na hivyo kuhifadhi sitara zao kwenye muktadha huo wa kimawasiliano.

**Mfano wa pili**

**Kikabarasi**

*Omanye valakaye vamalile kosi, lakini paka ndakutululakho matiti. Eyingovi yikhunulile ooh, ooh. Kuka vavola vari onyala okhwimichila amare badala yomukoye lakini kosi ni vutswa avana vefu , Kosi ni kavutswa, kosi namakhaya.*

**Ufafanuzi**

Katika usemi huu, mzungumzaji anasema kwamba, ingawa wanenaji watangulizi wamenena yote, lakini hatakosa la kunena. Anasema kuwa shetani amewanyang'anya kwa mshangao mkubwa.Anaendelea kusema kwamba akina babu walisema, "Unaweza kujinyonga kwa angalau mate badala ya kamba, lakini yote ni bure."

Usemi huu unaendana na kauli ya Brown na Levinson (1987) kwamba mbinu ya kutafuta ukubalifu huweza kutokea kwa njia ya kurudia maneno ambayo yamesemwa awali na watangulizi. Tunaona mzungumzaji akiwanukuu kina babu katika hotuba yake kwamba, "Kwa yale yaliyowakumba, mtu anaweza ghafilika hadi ajinyonge kwa mate, hata kama kamba itakuwa mbali." Kauli hii inampa ukubalifu kwa sababu wasikilizaji wanamuona kama mwombolezaji ambaye ameathiriwa kwa huzuni na majonzi kuliko wengine. Hii inampa nafasi ya kupitisha ujumbe wake kwa hadhira bila kuzuiliwa na kuhasiri sitara zake kimawasiliano.

**Kunadhibisha mnenaji na wasikilizaji kwenye tendo**

Mbinu hii ya mawasiliano inahusisha matumizi ya kiwakilishi cha nafsi ya pili wingi ("tu") ili kuwashirikisha wasikilizaji. Kulingana na Brown na Levinson (1987), matumizi ya nafsi ya pili wingi yanatafuta ushirikiano kwa kujidhibiti pamoja na wasikilizaji, hivyo kupunguza ulazima. Hii inaonyesha kwamba nafsi ya kwanza wingi haimaanishi wanenaji wengi wakisema kwa wakati mmoja, bali inatumika kushirikisha wazungumzaji na wasikilizaji katika muktadha wa mazungumzo. Tafiti hii iliweza kukutana na mifano kama vile;

**Mfano**

**Kikabarasi**

*Nikhwenya okhufura eliye lino mshivala shino avandu vefu, khuchendele halala.*
*Nikhuva ombu khunyala khwinjile mudini yindala nelitembeli lilala lia ovusangali nomulembe kwa Wele khakava.*

**Ufafanuzi**

Katika usemi huu, mzungumzaji anajiweka katika kundi moja na wasikilizaji kwa kusema kwamba, "Tukitaka kufaulu vita hivi, watu wetu, tutembee pamoja." Anaendelea kusema, "Ikiwa tunaweza, tujiunge kwa dini moja na kanisa moja la furaha na amani."

Mkakati huu unatumika hapa kwa sababu ya kuwaonyesha wasikilizaji kwamba mzungumzaji ako pamoja nao kwani yanayowakabili yanamkabili naye pia. Hii ni mbinu ya kuonyesha wasikilizaji kwamba wote wanashikilia kitu kimoja na hivyo kuhifadhi sitara za wasikilizaji. Hapa mzungumzaji anakwepa ulazima na kuwashawishi wasikilizaji kuingia katika chama kimoja na yeye kwa ajili ya kuleta umoja wa jamii na utengamano.

**Utumizi wa utambulisho wa vikundi**

Matumizi ya usemi kama "wapendwa wenzangu" na "laazizi wangu" katika mawasiliano yanaonyesha kuwa utofauti wa kimamlaka kati ya mzungumzaji na wasikilizaji ni mdogo au haupo, kulingana na Brown na

Levinson (1987). Mbinu hii inapunguza ulazima kwa kauli za mnenaji, ambapo badala ya kuamrisha, anawaomba wasikilizaji wazingatie usemi wake. Hali hiyo ilibainika katika hotuba za ibada ya mazishi, ambapo wananaji walichangia mawasiliano kwa kutumia ubadilishaji wa msimbo, majina ya kutukuza msikilizaji, na misimu.

**Mfano wa kwanza**

**Kikabarasi**

*Mshialo mno avana avaraka vashianje khuchendenje kaa sichila eshivalaa shino nishiavene. Baba vefu mwakhukama eliva lia oluyali ne mani khuvula shiekhumuelezia tawe khwalamsanditsanga vutswa ne Wele Khakavea mwene amlinde na makalusilie matanyi.*

**Ufafanuzi**

Mnenaji anasema kwamba, “Vijana wenzangu, tutembee polepole katika ulimwengu huu kwa sababu huu ulimwengu si wetu, ni wa wenyewe.” Anaendelea kusema, “Baba zetu walituonyesha tabia nzuri ya heshima, ila hatuna kitu cha kuwapa ila ni shukurani tu na kuwaombea baraka tele kutoka kwa Mwenyezi Mungu.”

Katika mazungumzo haya, tunaona matumizi ya neno “vijana wenzangu,” ambapo mnenaji anajaribu kuwarai kundi la vijana kwa kujihusisha nao ili waweze kumuona kama mwenzao na hivyo kumpatia muda wa kupitisha ujumbe. Hapa, mzungumzaji anafaulu kuwasiliana kwa sababu anatumia mbinu hii ya kuhifadhi sitara za wasikilizaji ambao ni vijana.Isitoshe, katika usemi wake, mnenaji anaendelea kwa kuwatambua kina baba na kuwamiminia sifa na hata kuwaombea baraka, maisha marefu, na yenye mafanikio. Kundi la wazee pia linafurahi na kuweza kumsikiliza mzungumzaji kwa kina na kumuunga mkono kwa usemi wake na kuyafanikisha mawasiliano.

**Mfano wa pili**

**Kikabarasi**

*Mama vefu muo…, Omanye bila enywe sikhwakhevulwe tawe. Lakini khuvulalili vywa omukho wa yikulu baba nyasaye wamulonga ne wamkama oluveleshelo lwokhuchinga omwana kachila nafwe khwavao. Vamasika imbinjilikha neindai sana, lakini machitso kamwimbinjilikha nako sikombakhanga tawe mulenjele sana efiayo fienyu …*

**Ufafanuzi**

Katika mazungumzo haya, mzungumzaji anatumia mkakati huu wa kimawasiliano kwa kuwatambua kina mama na kuwalimbikizia sifa kwamba, bila wao, watu hawangepatikana, maadamu ni wao walipewa uwezo wa kushika uja uzito, kuubeba, na hata kukoboa mtoto.

Mazungumzo haya, jinsi yalivyojitokeza kwenye ibada ya mazishi, yanawezesha mzungumzaji kuzinasa hisia za kina mama na hata kuhifadhi sitara zao kimawasiliano. Hivi kwamba, hata wanapoambiwa kwamba mafunzo wanayowapa wana wao, kama wameketi nao jikoni, hayajengi bali ni mafunzo ya kubomoa na kizivuruga akili zao, hawahisi kuwa wamedhalilishwa kiusemi na kitaadhima. Mbinu hii inawezesha kupitisha ujumbe mzito bila ugunduzi wa uzito wakati wa mawasiliano, bali ugunduzi huwa unaonekana baadaye na hata huenda usionekane kwa wasikilizaji wengine.

**Mfano wa tatu**

**Kikabarasi**

*Mukhulundi kuka wefu, omwami wayikholo yavatali, sijila niwe esilo yefu kakhulazimishanga mpaka kukhutechenie ne khandi khukhwitilekho. Esie kama mlomolomi wa yindalo ya vulano ndavolangendi yikhala mushifumbi isho notinyile maana orakalalekho. Karula mumunwa kukwo kave kokhulamilisia etsikhavi sijila omukhale yalomangari ovulime vywo omukhulundi vukwitsanga lulala sivukwitsanga khavili tawe.*

**Ufafanuzi**

Katika mfano huu, mzungumzaji anasema, “Babu yetu, kiongozi wa jamii ya vatali, ni wewe kigongo chetu ambacho tunajishikilia, inatubidi tukudekeze.” Anaendelea kusema, “Mimi kama mzungumzaji wa siku ya leo nasema kwamba kaa kwa hicho kiti bila wasiwasi wowote. Maneno yatokayo kinywani mwako yawe ya kutubariki, maadamu la mkuu ni dhahabu, bali si kinyume chake.”

Mazungumzo ya kumtambua na kuwatukuza viongozi yalisheheni ibaada za mazishi ambapo tuliweza kuchunguza kiini cha utambulisho huo kisha tukabainisha kwamba, wazungumzaji hutumia vitambulisho kama hivi kuhifadhi sitara zao na za jamii nzima kwani vyongozi wameteuliwa na jamii pana ambapo watu wengi ambao walishiriki kwe uteuzi huenda wamehudhuria hafla hiyo ya mazishi. Kulingana na Goffman (1967), kila mwanadamu anazo hisia za kuhifadhi sitara zake kwani sitara ni thamani ya kipekee ambayo Mwenyezi Mungu aliumba binadamu nayo kwa hivyo nisharti mawasiliano yaweze kuangalia au kutunza maslahi ya sitara. Wazungumzaji hutumia mikakati hii ya upole kimawasiliano kwa nia ya kunasa hisia za wasikilizaji na kusistiza mawazo yao kwa jamii pana kimawasiliano.

**Kutoa ahadi kwa wasikilizaji**

Ahadi ni mambo ambayo yanawafunga wazungumzaji katika utekelezaji wa mambo katika siku zijazo, kulingana na Austin (1962). Matumizi ya ahadi katika mazungumzo ni mkakati wa upole wa chanya unaoepuka kuharibu sitara za wasikilizaji, kama ilivyoelezwa na Brown na Levinson (1987).

**Mfano wa kwanza**

**Kikabarasi**

*Vafwililwe, vamasika nende avacheni vosi vetsile okhukhutila omukoye munda, mlembe vosi, mlembe khadi? Ndenyanga okhumusuvilisia yindalo ya vulano endi mlamwa okhwenda tawe ndakholakho kenyala solakona yinzala tawe. Munzu mwa omwana wefu eliosi lilendelea okhuvuya olalia, olanywa ne khandi olesinga.*

**Ufafanuzi**

Waliofiwa, wenye matanga, na wageni wote ambao wamekuja kutufunga mkanda, hamjambo nyote, hamjambo tena? Nataka kuwahakikishia siku ya leo kwamba, Shemeji, usiwe na wasiwasi, nitafanya niwezalo, hautalala njaa. Hapa kwako mapishi yataendelea, utakula, utakunywa, na tena utaoga.

Katika mazungumzo haya, mnenaji anatoa ahadi kwamba atailinda aila ya nduguye mwendazake kupitia juhudi zake. Tunaona akipeana ahadi kwenye hotuba yake katika ibaada ya mazishi. Ahadi ambayo itamlazimu kujikakamua ili aweze kutimiza. Mbinu ya wazungumzaji kujifunga kwa ahadi tekelezi huwezesha uhifadhi na udumishaji wa sitara za wasikilizaji haswa walofiwa kwenye ibaada mzishi hivyo basi kumwezesha mzungumzaji kukamilisha hotuba yake bila kuzuiliwa na waombolezaji.

**Upole Hasi katika ibaada ya Mazishi katika lugha ya Kabarasi**

Mikakati ya upole hasi inatumika wakati wazungumzaji wanazungumza kwa kuepuka kulazimisha wasikilizaji, kwa kutumia kauli za lugha ya upole. Ni hali ya wasikilizaji kujipa uhuru wa kufanya yanayomfurahisha bila kizuizi chochote kimawasiliano (Brown & Levinson, 1987). Mikakati hiyo inahakikisha kuwa sitara hasi za msikilizaji zinadumishwa bila kuingiliwa, na haikusudii kuingilia matendo yake. Katika ibada za mazishi katika vitongoji vya Kaunti Ndogo ya Kakamega Kusini, Jimbo la Kakamega, mikakati ya upole hasi inatumika kuhifadhi sitara za wasikilizaji kwa njia zifuatazo.

**Kuwa na chukulizi zilizochache juu ya malengo ya msikilizaji**

Katika mbinu hii, wazungumzaji hawana uhakika kuhusu vitendo vya wasikilizaji, hivyo wanapaswa kuwa waangalifu ili kuepuka ulazima.

**Mfano;**

**Kikabarasi**

*Vamasika vosi, khunyala okhuva nomundu walenyanga okhukalukha hango hano yenone omulembe kwa avana va owashiefwe aleshile…? Esie sembara tawe, sichila fwesi khwalenyanga avana vano vave no omulembe muvulamu vwavo.*

**Ufafanuzi**

Waombolezaji wote, tunaweza kuwa na mtu yeyote ambaye anatazamia kuja kuvuruga amani ya watoto wa marehemu? Kwangu mimi, sidhani, maana sisi sote tunataka watoto hawa waishi kwa amani katika aushi yao.

Katika usemi huu, mzungumzaji hataki kuhasiri sitara za wasikilizaji kwa kudokeza wazi kwamba watu ambao wanatazamia kurudi kwa familia ya marehemu kwa nia ya kumridhi mjane na kuivuruka amani ya watoto yatima wasidhubutu. Hii inasaidia kwa kuwezesha mawasiliano na kunasa hisia za wasikilizaji, kwani pindi wasikilizaji

wanatarajia mnenaji adokeze wazi kwamba wanaume wanaokusudia kuvuruga amani miongoni mwa waombolezaji wakome na wasijaribu kuonekana kijijini kwa malengo kama hayo.Mzungumzaji anaonyesha kuwa na chukulizi chache na kijalizo kwamba wote ni watu ambao wana nia ya kuboresha na kuendeleza ama kwa ajili ya familia iliyoachwa na mwenda zake. Kwa hivyo, mikakati hasi ya upole inawapa wasikilizaji hakikisho la kuwa na uhuru wa kuyafanya mambo yanayowafurahisha bila kuulizwa maswali au kuhitaji ruhusa ya kuuliza maswali.

**Utumizi wa kauli ambazo ni za kijumla ambazo haziwarejelei watu maalum**

Hapa wazungumzaji hukwepa utumiaji wa viwakilishi nafsi kwa msikilizaji ambapo wazungumzaji huweza kuhifadhi sitara za msikilizaji kwa kuhepa kumrejelea kwa njia ya moja kwa moja Mnenaji huwa analenga vitendo vyenyewe zaidi ya wanaorejelewa. Kauli hii inatokeza maana kwamba, matumizi ya nafsi ya pili kwenye mawasiliano kwa wakati mwingine hayawezi kuwezesha utambulisho wa msikilizaji kwa njia iliyowazi kwani haichulikani moja kwa moja ni nani haswa mzungumziwa katika matamshi ambayo ni ya kijumla.

**Mfano**

**Kikabarasi**

*Avashiefwe mukhumililanga mutsinyali lukano na lukano, nimuyanza mukhwivalile oluyali khonafwe khulonde ka mwalenyanga okhurula mumechitso kenyu. Omanye ninywe esura yeshikwenyi shino komukhola kosi kalachoranga eshikwenyi shiosi, nimuloka fwesi khuva khulochile ne nimwilatsa evanjeli khandi khuvetsanga khwilwatsile fwesi.*

**Ufafanuzi**

Wenzetu mnaotuongoza katika vitengo mbalimbali, mkipenda mtuonyeshe heshima ili sisi tuweze kufuata mambo ambayo mnataka kutoka kwa mafundisho yenu. Mjue kwamba nyinyi ndio sura ya kitongoji hiki; yote mnayoyafanya yanaonyesha sura ya kijiji kizima, halafu inakuwa chukulizi kwamba ni tabia ya wanakijiji. Mkiroga, ni sisi sote tumeroga, na mkihubiri Biblia, tena ni sisi sote kama wanakijiji tunaohubiri neno la Mungu.

Kauli kama "wenzetu wanaotuongoza kwenye vitengo mbalimbali" ni kauli ya kijumla ambayo haulengi mtu mmoja. Kwa hivyo, hata ikiwa na machungu ambayo yanaweza kuhasiri sitara za msikilizaji, yameweza kudhibitiwa kwa kujumuisha wanakitongoji wote, kwani hauonyeshi mtu mahususi ambaye mzungumzaji analenga katika ujumbe wake.Isitoshe, matumizi ya maneno kama "sisi sote kama wanakitongoji" ni mbinu ya kugawanya tuhuma au fadhila kwa watu wengi, hivyo basi sitara za wasikilizaji zinahifadhiwa kimawasiliano. Mikakati hii ya upole ni mikakati ambayo inaweza kuchangia uhifadhi wa sitara za watu wengi kiujumla na hata mtu mmoja kibinafsi.

**Mbinu ya kuonyesha wasikilizaji taadhima**

Matumizi ya mikakati hasi ya upole huwezesha mzungumzaji kuepuka kuingilia faragha na uhuru wa wasikilizaji kwa utumizi wa lugha na matendo yanayoonyesha taadhima kwake msikilizaji (Brown na Levinson 1987). Mawazo haya yanakubaliana na kauli ya Leech (1983) ambaye anapendekeza mkakati wa kujitweza kama mkakati wa kuhifadhi sitara za msikilizaji katika mazungumzo. Hivi kwamba, badala ya mzungumzaji kujisifu kimawasiliano, anajidunisha na kummiminia sifa msikilizaji na kumfanya ahisi vyema.

Wanenaji huwa wanatumia nyimbo kwenye hotuba zao katika ibaada ya mazishi ili kuonyesha heshima kwa mwenda zake pamoja na waliompoteza au familia ya mwenda zake.

**Kwa mfano**

**Kikabarasi**

*Omulina wanje omulina wanje… Mulina wanje umbakale…*
*Omukosi waje omukosi wanje … Mkosi wanje umbakale…*
*Omwechitsi wanje omwechitsi wanje… Mwechitsi wanje umbakale…*

**Ufafanuzi**

Katika mfano huu, mnenaji anaamua kuutumia wimbo ambao unaashiria kwamba mwenda zake alikuwa rafiki yake na amemwanika kwa kuipiga dunia tege au kuaga dunia.Mbinu hii ya kimawasiliano ni mbinu ambayo inawapatia waombolezaji fadhila pamoja na urejesho kwamba si wao pekee waliopoteza, ila hata wengine kama mzungumzaji wameweza kupoteza rafiki.

Mkakati huu unatoa mchango katika mawasiliano kwa kunasa hisia za wasikilizaji na kumuunganisha mzungumzaji na jamii ya mwenda zake. Hata hivyo, mbinu hii inawezesha uhifadhi wa sitara za wasikilizaji, hususan familia ya mwenda zake.

**Utumizi wa mkakati ndani ya rekodi kwenye usemi wa kimawasiliano**

Mkakati huu wa upole kimawasiliano huwa unatumika wakati mnenaji anamzungumza kwa kumrejelea msikilizaji moja kwa moja kwa nia ya kumjulisha mahitaji yake. Hivyo basi, nia ya matumizi ya mkakati huu si kupunguza vitisho kwa sitara za msikilizaji bali ni kufikisha jumbe jinsi ulivyo (Brown na Levinson 1987). Hata hivyo, mkakati huu wa kimawasilisiliano hutumika zaidi miongoni mwa watu ambao wana uhusiano wa karibu.

**Mfano wa kwanza**

**Kikabarasi**

*Avalomolomi vasikale nimyanza mukhatsia amakhuva amanyinji tawe, mukhukhonye etsisa tsilovile.*

**Ufafanuzi**

Mzungumzaji anawaambia kwamba wanenaji waliobaki wasiongee maneno mengi, wasaidie kuokoa muda.

Katika usemi huu, mnenaji anatoa kauli kwamba "msizungumze mengi" kuonyesha kwamba hana haja ya kutumia lugha ya upole, kwani wazungumzaji ambao wamebaki kwa ratiba ya mazungumzo ni watu wa ukoo wake na wana uhusiano wa karibu naye. Kwa hivyo, hawezi kuhasiri sitara zake kwa kuwaamrisha waongee maneno machache.

**Mfano wa pili**

**Kikabarasi**

*Senje vola tse elira ne mutsie mwikhale, nomba mwimbe tsolwimbo.*

**Ufafanuzi**

Shangazi, sema tu jina, halafu mrudi kuketi au muimbe tu wimbo.

Katika mazungumzo haya, mzungumzaji anatumia amri kwa kuwaamrisha shangazi zake kwamba wasiongee, bali wajitambulishe tu kwa jina kisha warudi kuketi au waimbe wimbo. Mazungumzo haya yanaonyesha uhusiano wa karibu ambapo, hata akiongea kwa kuamrisha, sitara za wasikilizaji hazitadhurika. Mkakati huu, hivyo basi, unatumika kwenye hafla kama hizi kuokoa muda.

**Utumizi wa mkakati nje ya rekodi au tamko fiche kwenye mawasiliano**

Hapa mzungumzaji huwasilisha jumbe kwa namna fiche, yaani maana ya jumbe haijitokezi bayana. Mkakati huu wa kimawasiliano huwezesha mzungumzaji kuepuka lawama kisha sitara zake na za msikilizaji zinahifadhiwa. Yule (1996) anadai kwamba matumizi ya mkakati huu wa mawasiliano huweza kutatiza ufasiri wa ujumbe kwani, msikilizaji huenda asiweze kufasiri maana kusudiwa kwenye mawasiliano labda kama kuna umaanisho fulani kwenye usemi huo. Wazungumzaji kwenye ibaada ya mazishi waliupitisha ujumbe wao kupitia mbinu zifuatazo;

**Utumizi wa maswali yasiyohitaji majibu**

Wakati mwingine, wanenaji hutumia maswali ya balagha kupitisha ujumbe wao kwa umati kwa nia ya kunasa hisia za wasikilizaji na hata kuepuka kuhasiri sitara za wasikilizaji wao kimawasiliano.

**Mfano**

**Kikabarasi**

*Avandu vanje niwina wamanya eyindalo yiye yokhufwa? Chende khukalushile Wele sichila niye yenyene umanyanga makhuva komwana womundu.*

**Ufafanuzi**

Maneno haya katika lugha ya Kiswahili yana maana kwamba, "Watu wangu, ni nani anayejua siku ya kufa kwake?" Anaendelea kusema, "Tumrudie Mungu, maadamu Yeye ndiye aliyejua mambo ya binadamu."

Mzungumzaji anatumia mbinu hii kwa kuuliza waombolezaji ikiwa kuna anayejua siku ya kifo chake. Bila kungoja jibu, anawafahamisha kwamba ni bayana kuwa hakuna mtu yeyote anayejua siku yake ya kufa, kisha anawahimiza waichukue njia ya kumfuata Mungu kwa kumwabudu, maadamu ni Yeye pekee aliye na uwezo wa kujua aushi ya binadamu. Hata hivyo, mzungumzaji hataki kuwakashifu watenda dhambi moja kwa moja kwa sababu hakusudii kuhasiri sitara zao kimawasiliano.

**HITIMISHO NA MAPENDEKEZO**

**Hitimisho:** Katika utafiti huu, imebainishwa kuwa wazungumzaji katika ibada za mazishi wanaotumia lugha ya Kikabarasi hutagusana kwa kutumia mikakati ya upole ili kuhifadhi sitara za wasikilizaji katika mawasiliano. Utafiti huu umezingatia mchango wa mikakati ya upole katika mawasiliano ya ibada za mazishi kwa lugha ya Kikabarasi katika Kaunti Ndogo ya Kakamega Kusini, iliyopo katika Jimbo la Kakamega, Kenya. Imegunduliwa kuwa wazungumzaji hutumia mikakati ya upole katika mawasiliano kwa lengo la kunasa hisia za wasikilizaji na kuhifadhi sitara zao. Mikakati ya upole iliyochunguzwa ni pamoja na mikakati ya upole wa chanya, mikakati ya upole hasi, mikakati ndani ya rekodi, na mikakati nje ya rekodi au matamko fiche.Utafiti huu utasaidia wasikilizaji na waombolezaji kupata maarifa na ustadi wa kuwahutubia watu wa tabaka mbalimbali katika hafla za jamii changamano. Aidha, utafiti huu utachangia kuongeza data katika uga wa isimu kwa kutoa makala ya urejelezi wa kiusomi kiufundi, na hivyo kuboresha ujifunzaji na ufundishaji wa taaluma za isimu.

**Mapendekezo:** Utafiti huu unapendekeza kwamba kwa kuzipa mianya ya kiusomi, uvumbuzi kuhusu changamoto zilizopo katika matumizi ya mikakati ya lugha ya upole kwenye mawasiliano hususan katika hafla za sherehe ya kumbukumbu ya mashujaa nchini unahitajika na hata katika Jukwaa la Facebook.

**REFERENCES**

Adewale, K. A., & Taofeek, O. A. (2018). Politeness and discourse functions in doctor-patient verbal interaction at the University College Hospital, Ibadan, Nigeria. *International Journal on Studies in English Language and Literature, 6*(12), 1–12.

Austin, J. L. (1962). *How to do things with words*. Oxford University Press.

Brown, P., & Levinson, S. C. (1978). Politeness: Some universals in language use: Politeness phenomena. In E. Goody (Ed.), *Questions and politeness*. Cambridge University Press.

Brown, P., & Levinson, S. C. (1987). *Politeness: Some universals in language usage*. Cambridge University Press.

Kioko, N., & Mavisi, R. M. (2021). Mikakati ya upole katika mawasiliano ya wahudumu wa magari ya uchukuzi na abiria katika lugha ya Kikamba. *Jarida la Isimu Jamii*.

Leech, G. (1983). *Principles of politeness*. Longman.

Mashiri, P. (2001). Managing face in urban public transport: Polite request strategies in commuter omnibus discourse in Harare, Africa. *Zambezia, 28*(1), 85–94.

Muge, T. (2018). *Uchanganuzi wa upole katika mazungumzo ya vipindi vya Sobetab Kapchi katika idhaa ya Kass FM* (Master's thesis). Moi University.

Njambi, C. (2010). *An analysis of politeness strategies in Gikuyu: A case of Thika sub-county, Kenya* (Master's thesis). Kenyatta University.

Yule, G. (1996). *Pragmatics*. Oxford University Press.